# DARASA LA SITA

**KISWAHILI**
**SEHEMU YA KWANZA:**
**LUGHA**

**Muda: Saa 1 dakika 40**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi.***

Kuna aina mbalimbali ___1___ matunda. Mifano ya miti ya matunda ni miembe, michungwa na ___2___. Matunda ___3___ huwa na sukari ___4___ ingawa baadhi huwa hayana; lakini yote ni muhimu mwilini. Mtu ___5___ matunda mara kwa mara hujiepushia ___6___ maradhi mengi. Mbali na matunda, ni ___7___ pia ___8___ maji ya kutosha. Maji husaidia ___9___ uchafu mwilini.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. ya | B. la | C. za | D. na |
| **2.** | A. mikarafuu | B. mitufaha | C. miwa | D. shayiri |
| **3.** | A. mengine | B. mingine | C. zingine | D. ingine |
| **4.** | A. mengi | B. mwingi | C. jingi | D. nyingi |
| **5.** | A. anayeyakula | B. alaye | C. anayezikula | D. anakula |
| **6.** | A. kushika | B. kugonjeka | C. kuugua | D. kuungua |
| **7.** | A. mzuri | B. kuzuri | C. nzuri | D. vizuri |
| **8.** | A. kuyanywa | B. kukunywa | C. kunywea | D. kuyakunya |
| **9.** | A. kutowa | B. kuondoa | C. kutia | D. kuweka |

Timo ___10___ mvulana mkaidi ___11___ hakuwatii wala ___12___ walimu wake. Aliadhibiwa kila siku lakini akawa sikio la kufa ambalo halisikii ___13___. Tatizo ___14___ kwamba wazazi wake walimdekeza wakati ___15___ bila kumwonyesha madhara ya tabia zake.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. atakuwa | B. amekuwa | C. alikuwa | D. alikua |
| **11.** | A. ambayo | B. ambapo | C. ambako | D. ambaye |
| **12.** | A. kuwaheshimu | B. kumheshimu | C. kutuheshimu | D. kukuheshimu |
| **13.** | A. neno | B. dawa | C. kitu | D. uchungu |
| **14.** | A. ilikuwa | B. yalikuwa | C. alikuwa | D. lilikuwa |
| **15.** | A. yote | B. yoyote | C. wote | D. wowote |

**Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com**

**Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.**

16. Chagua tashbihi iliyokamilishwa ipasavyo.
    A. Mwaminifu kama mchana.
    B. Mjinga kama mlingoti.
    C. Mtukutu kama mbuzi.
    D. Mwembamba kama twiga.
17. Kiatu chake kimeraruka **vibaya**. Neno lililopigiwa mstari ni aina ya:-
    A. Kivumishi
    B. Kiunganishi
    C. Kielezi
    D. Kitenzi
18. Sehemu gani hupatikana kwenye kiwiliwili?
    A. Kidakatonge
    B. Muundi
    C. Ndewe
    D. Nyusi
19. **Bunda** ni la noti na **tita** ni la
    A. maji
    B. nzige
    C. nafaka
    D. kuni.
20. **Andika wingi wa sentensi ifuatayo.**
    `  :a ameenda dukani.
    A. Wamama wameenda dukani.
    B. Akina mama wameenda dukani.
    C. Wamama wameenda madukani.
    D. Akina mama wameenda madukani.
21. **Kamilisha kwa kiashiria radidi.**
    Kuimba _____ ndiko kulikotufurahisha.
    A. huku huku  B. kuku kuku
    C. kuku huku  D. huku kuku
22. Kutokana na nomino **'mkulima'** tunapata kitenzi gani?
    A. Kilimo  B. Lima
    C. Ulimaji  D. Ukulima
23. Ni kitenzi kipi kinachoonyesha kauli ya **kutendwa**?
    A. Fugwa  B. Pika
    C. Chezea  D. Inuka
24. **Ni sentensi gani iliyo sahihi?**
    A. Wao ndiyo waliofika mapema.
    B. Sisi ndisi tulioalikwa.
    C. Wewe ndiye utakayemsaidia.
    D. Nyinyi ndio mliopongezwa.
25. **Tegua kitendawili kifuatacho:**
    Huku mwamba na huko mwamba.
    A. Giza  B. Nazi
    C. Kaburi  D. Pango
26. **Kanusha:**
    Kuja kwake kulitufurahisha.
    A. Kutokuja kwake kulitufurahisha.
    B. Hakuja wala kutufurahisha.
    C. Asipokuja hatatufurahisha.
    D. Kutokuja kwake hakukutufurahisha.
27. Ni neno lipi halionyeshi aina ya kimelea?
    A. Siafu  B. Chawa
    C. Kupe  D. Utitiri
28. Chagua sentensi yenye `  :ha masharti.
    A. Mama alifua nguo akiimba.
    B Kikombe kilichoumia kimetibiwa.
    C. Kikombe hicho ni kichafu
    D. Mkisoma kwa bidii mtafaulu.
29. Tarakimu **100000** kwa maneno ni:-
    A. milioni moja  B. laki moja
    C. elfu kumi  D. laki mia moja
30. Chagua methali inayowahimiza watu wafanye mambo taratibu.
    A. Ngoja ngoja huumiza matumbo.
    B. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.
    C. Haraka haraka haina baraka.
    D. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali 31-40.***

Niliazimia kubaki ili niwanase samaki. Wavuvi wenzangu walikuwa wamerejea makwao mikono mitupu.

**Nilipiga moyo wangu konde** na kujiambia moyoni, "Na liwe liwalo." Nyavu zilikuwa majini na nilipojaribu kuzivuta nilihisi uzito fulani uliofanya moyo wangu kufurahi.

Nilianza kuzivuta nyavu zile, nikavuta na kuvuta. Ajabu ni kuwa uzito ule ulikuwa ni kama wa nanga. Sikufa moyo. Nilijaribu kwa mara ya pili na nilipokuwa karibu kupata ushindi, nilijihisi nikivutwa kwa nguvu ambazo sikuwa naziona na kisha nilitupwa majini.

Nilipiga unyende na wakati huo, mlizamu wa maji ulipata nafasi kuingia kinywani mwangu. Nilijipata nimeshikwa mkono na majitu mawili ambayo yalikuwa na jicho moja na kinywa kimoja kilichotoa moto.

Majitu yalikuwa yakitoa sauti ya kuguna na kunguruma ambapo nilifahamu kwamba yalikuwa yakiwasiliana. Yalinipeleka katika chumba kikubwa kule chini ya bahari. Chumba hiki kilikuwa kimenakshiwa kwa dhahabu, hasa ukutani. Sakafu ilikuwa imenakshiwa kwa shaba.

Katika chumba hiki, kulikuwa majitu mengine na kilichonitia hofu zaidi ni mfalme wa majitu aliyekuwa tofauti na wenzake kiasi kidogo. Alikuwa mkubwa zaidi na mwenye macho matatu, vinywa viwili na miguu minne.

Wakati huu, nilianza kuwakumbuka wavuvi wenzangu. Nilikumbuka mke wangu Halima na watoto wangu Juma na Fatuma. Laiti ningewasikiliza wavuvi wenzangu haya yasingenipata. Nilipokuwa nimezama katika lindi la mawazo, nilihisi nimenyanyuliwa juujuu na mojawapo ya majitu hayo. Kulikuwa na pipa kubwa lenye maji yakichemka. Kwa mwendo wa madaha, Jitu hili liliniinua huku mengine yakishangilia na kunielekeza pipani humo. Liliniachilia nikiwa hewani. Nilijiona nikirudi chini kwa kasi huku kichwa changu kimelenga mlango wa pipa la maji moto. nikapiga mayowe.

Hapo ndipo nilipogutuka kutoka usingizini. Mwili wangu ulikuwa umezizima, huku nimelowa jasho. Moyo ulinidunda dududu. Ndipo nilipong'amua kwamba lilikuwa **jinamizi** tu!

**31.** Changua jibu sahihi.
- A. Mwandishi aliamua kuwa hatatoka nyumbani.
- B. Mwandishi alinasa samaki wengi siku hiyo.
- C. Wavuvi walienda nyumbani bila samaki.
- D. Wavuvi walienda na samaki wengi siku hiyo.

**32.** Msemo **'nilipiga moyo konde'** unaonyesha kuwa msimulizi:-
- A. alijipiga ngumi
- B. aliamua kujitahidi
- C. aliogopa sana
- D. hakujali chochote.

**33.** Moyo wake ulifurahi wakati:-
- A. alipozihisi nyavu kuwa nzito
- B. alipowaona samaki wengi
- C. alipozitoa nyavu majini
- D. alipovua samaki mzito.

**34.** Msimulizi alipogundua kuwa nyavu zilikuwa na uzito wa nanga:-
- A. aliacha kuzifuta
- B. aliogopa sana
- C. aliendelea kuzivuta
- D. alipiga unyende.

**35.** Baada ya kupiga unyende mwandishi:-
- A. alitema maji
- B. alitapika maji mengi
- C. alianza kuvutwa
- D. aliingiwa na maji kinywani.

**36.** Jibu lipi ni kweli kuhusu chumba alichopelekwa mwandishi?
- A. Kilikuwa na kuta za shaba.
- B. Sakafu ilikuwa ya dhahabu.
- C. Kuta zilirembeshwa kwa vigae.
- D. Kuta zilirembeshwa kwa dhahabu.

**37.** Kuguna na kunguruma kwa majitu:-
- A. ilikuwa ni njia ya kuwasiliana
- B. hakukumtisha mwandishi
- C. kulitokana na ukubwa wao
- D. ilikuwa njia ya kumchezea mwandishi.

**38.** Tofauti ya mfalme na majitu mengine ilikuwa yafuatayo **isipokuwa**:-
- A. ukubwa wake
- B. macho matatu
- C. vinywa vitatu
- D. miguu minne.

**39.** Kilichomfanya msimulizi kujuta ni:-
- A. kumkumbuka mkewe Halima
- B. kupuuza maneno ya mvuvi.
- C. kutupwa kwenye pipa la maji
- D. kumkumbuka mwanawe Fatuma.

**40.** **'Jinamizi'** kulingana na makala ni nini?
- A. Usiku wa ajabu.
- B. Ndoto njema.
- C. Jambo la aibu.
- D. Ndoto ya kutisha.

**Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali kuanzia 41 mpaka 50.***

Kila binadamu alijipata akiwa mzaliwa mahali fulani duniani. Hakuna yeyote aliyetoa ruhusa ya kuzaliwa popote pale. Leo hii, nchini tulimo, hatukuchagua kuzaliwa humo na kwa hivyo tunahitajika kutunza na kuipenda nchi yetu. Huu ndio unaoitwa **uzalendo**.

Uzalendo ni upendo wa dhati kwa nchi yetu. Mzalendo halisi ni yule aliyetayari kulinda nchi yake kwa udi na uvumba. Mzalendo huwa tayari hata kufia nchi yake ikiwezekana.

Wananchi wazalendo ndio nguzo ya nchi. Ubinafsi huwa mbali nao na hujitolea kusaidia wengine bila kuonyesha kujipenda. Aliye na upendo wa dhati kwa asili yake huwa na maingiliano mazuri, na maadili mema ni kishawishi cha utendaji mema katika jamii. Wengine huvutiwa na vitendo vyake na kutaka kuwa kama yeye. Wananchi wazalendo ni rasilimali imara ya nchi. Wananchi hawa hufuata sheria za nchi kikamilifu.

Nchi ya Kenya imekuwa na wazalendo ambao walihatarisha maisha yao na hata kufa ili kuilinda nchi hii. Mashujaa kama Dedan Kimathi, ambao hata hawakuonja tunda la uhuru, walikufa ili tupate uhuru kutoka kwa Wakoloni. Wengine walimwaga damu na wengine ambao kwa sasa wako hai walipigania nchi hii bila kuonyesha hisia za ubinafsi. Watu wa aina hii ndio wanaofanya taifa lidumu.

Aliye mzalendo wa kweli **huyapa maslahi ya nchi kipaumbele** kuliko yake mwenyewe. Ikiwa kuna uchaguzi, kwa mfano, hakutazuka vita vyovyote kwa kuwa wazalendo hawataiba kura. Uchaguzi utakuwa wa haki na kila mmoja atakuwa ametosheka na kuukubali. Taifa kama hili hukua kiuchumi, kijamii na kisiasa. Ufisadi huwa haupo kwa kuwa hili ni zao la ubinafsi.

Kwa upande mwingine, dhana ya uzalendo haimaanishi kuwa na chuki kwa mataifa mengine au watu wasio wa asili yako. Uzalendo ni kuendeleza upendo kwa kila binadamu na watu kuwa tayari kutumikia wengine. Kwa njia hii tutakuwa na dunia isiyo na vita vyovyote. Tutafurahia kokote tuendako kwa kuwa kuna usalama na upendo. Kwa hakika, tukizingatia uzalendo, dunia itakuwa pahali pema pa kuishi, maskini hawatakuwa kati dunia kila mmoja atakuwa na maisha mazuri.

**41.** Ni kweli kuwa:-
- A. mtu huzaliwa pale apendapo
- B. wengi huzaliwa kule wasikopenda
- C. mtu hawezi kuishi pale atakapo
- D. mtu hana hiari ya pale atakapozaliwa.

**42.** **Uzalendo** ni nini?
- A. Mtu anayeipenda nchi yake.
- B. Ni hali ya kuzaliwa katika nchi.
- C. Ni hali ya kutunza na kuipenda nchi yetu.
- D. Ni hali ya kufia katika nchi yako.

**43.** Ni ipi si tabia ya mzalendo?
- A. Kuilinda nchi yake.
- B. Kuwasaidia wengine.
- C. Kusaidiwa na wengine.
- D. Kuzingatia maadili.

**44.** Mtu akiwa na matendo mazuri:-
- A. huigwa na wengine
- B. huwaiga wengine
- C. hupendelea wengine
- D. huchukiwa na wengine.

**45.** Sheria zinapowekwa nchini, wazalendo:-
- A. huzipinga
- B. huzifuata
- C. huzikaidi
- D. huziogopa.

**46.** Kulingana na aya ya nne:-
- A. wazalendo walihatarisha maisha ya wakenya
- B. baadhi ya watu hawakuuona uhuru waliopigania
- C. mashujaa waliotajwa bado wako hai
- D. mashujaa wote waliopigania uhuru walikufa.

**47.** Kupigania nchi kunaonyesha kuwa mashujaa:-
- A. hawakujipenda kuliko wengine
- B. hawakuipenda nchi
- C. walipenda kumwaga damu
- D. hawakuwa wazalendo.

**48.** **Kuyapa maslahi ya nchi kipaumbele** ni:-
- A. kutojali nchi
- B. kujijali kwanza
- C. kupenda nchi za wengine
- D. kujali nchi kwanza.

**49.** Nchi huweza kuimarika kiuchumi iwapo:-
- A. mtu hatajali mambo yake kwanza
- B. haki na uzalendo zitadumishwa
- C. watu watazingatia ufisadi na uchaguzi huru
- D. viongozi wote watashinda uongozi wao.

**50.** Kichwa mwafaka zaidi kwa makala haya ni:
- A. Mashujaa wa uhuru.
- B. Nchi yenye wazalendo.
- C. Umuhimu wa uzalendo.
- D. Mahali pema pa kuishi.

**Compiled and supplied online by Schools Net Kenya | P.0.Box 85726-00200, Nairobi. Tel:+254202319748 | +254733836593 | email: infosnkenya@gmail.com. Order answers online at: www.schoolsnetkenya.com**